

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Anwani ya Simu: "ELIMU" Simu:
026 296 35 33
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 10,
40479 DODOMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. GA.80/145/01A/57

21 Novemba, 2024.

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P. 2662,
DODOMA.

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P. 1454,
DAR ES SAALAM.

Katibu Mtendaji,
Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P. 21422,
DAR ES SAALAM.

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Inventors in Education (TAPIE),
S.L.P. 13346,
DAR ES SAALAM.

Mwenyekiti,
Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA),
S.L.P. 8581,
DAR ES SAALAM.

Mkurugenzi,
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),
S.L.P. 13547,
DAR ES SALAAM.

Mwenyekiti,
TAWOSCO,
S.L.P. 2458,
DODOMA.

Umoja wa Wazazi Jumuiya ya CCM,
S.L.P.3,
DODOMA.

WARAKA WA ELIMU NA. 03 WA MWAKA 2024 KUHUSU
KALENDA YA MIHULA YA MASOMO KWA SHULE ZA AWALI, MSINGI NA
SEKONDARI MWAKA 2025

Tafadhali rejea kichwa cha habari.

2. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na idadi sahihi ya siku za masomo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa **Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa mwaka wa masomo 2025.**
3. Ni muhimu kuzingatia utekelezaji wa Kalenda husika kwa ufanisi ili kuepuka changamoto ya kutokamilisha ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote kwa wakati na hivyo kulazimika kuweka mipango ya ufundishaji na ujifunzaji inayowanyima watoto/wanafunzi fursa ya kupumzika na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii katika familia na jamii zao.
4. Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Awali, Msingi na Sekondari kwa mwaka 2025 ni kama ifuatavyo:

MIHULA	KUFUNGUA MUHULA	LIKIZO FUPI		KUFUNGA MUHULA	IDADI YA SIKU ZA MASOMO
		KUFUNGA	KUFUNGUA		
Muhula I	13/01/2025	11/04/2025	22/04/2025	06/06/2025	98
Muhula II	08/07/2025	29/08/2025	15/09/2025	05/12/2025	96
Jumla ya Siku za Masomo					194

Tanbihi:

- Siku za Masomo kwa mwaka ni **194**.
 - Mashindano ya UMITASHUMTA yatafanyika tarehe 08/06/2025 hadi 21/06/2025, na UMISSETA yatafanyika tarehe 22/06/2025 hadi 04/07/2025.
 - Mashindano ya Michezo ya Shule za Sekondari za Afrika Mashariki (FEASSSA) yatafanyika tarehe 17/08/2025 hadi 29/08/2025.
 - Ili kupunguza muda mwingi wa mapumziko kwa wanafunzi ambao unaweza kuathiri ratiba za masomo, na kwa kuzingatia kuwa mwaka ujao ni mwaka wa uchaguzi, Kamishna wa Elimu amelazimika kufanya maboresho katika Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa mwaka 2025 kama ilivyokuwa imewasilishwa awali.
5. Kutokana na maboresho hayo, Waraka huu unafuta Waraka Na. 02 wa Mwaka 2024 uliotolewa na kusambazwa wenye **Kumb. Na. GA.80/145/01A/56** wa tarehe 8 Novemba, 2024.
 6. Nawatakia utekelezaji mwema.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
KAMISHNA WA ELIMU

Nakala: Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Kanda na Wilaya,
TANZANIA BARA.

Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania.



**Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi,
Jitokeze Kushiriki Uchaguzi**